umaskini uliokithiri, kutengwa, ugumu wa upatikanaji wa huduma za kijamii, ukosefu wa ajira na ukosefu wa fursa za kujikimu na kushindwa kuchangia katika uchumi wa taifa.

**DIGNITY Kwanza** tunaamini kwamba haki za watu zikilindwa, kila kitu kitajiweka mahala pake, hiyo ndiyo ‘’**DIGNITY Kwanza**’’.

## MAADILI YETU YA MSINGI

1. **Tunaheshimu Utu:** Tunatumia njia ya haki za binadamu katika mashirikiano yetu na wanufaika wa huduma zetu.
2. **Tunaamini katika tunachokifanya.** Tunazingatia maadili ya kazi (Uadilifu, uwajibikaji, taaluma na uwazi) katika kuendesha shughuli zetu.
3. **Tunathamini nafasi ya kufanya mabadiliko chanya katika maisha ya watu**: Tunafanya nao kazi na kutambua kwa pamoja changamoto na kutafuta suluhisho endelevu
4. **Sisi ni suluhisho endelevu; tunaamini katika ubunifu na ujasiri:** Hatukati tamaa kwa urahisi, hata katika hali ngumu zaidi tunatafuta ufumbuzi/majibu ya changamoto.
5. **Tunawajali wafanyakazi wetu - tunaunda na kukuza utamaduni ambao unawawezesha wafanyakazi wetu kuwa na afya njema:** Usawa wa maisha, maendeleo ya kazi na maisha bora.
6. **Tunathamini utofauti wetu:** Tunatumia fursa ya kujifunza mawazo mapya kwa wale walio tofauti na sisi na kuwashirikisha katika maadili yetu.
7. **Tunawatambua na kuwathamini washirika wetu:** Tunaheshimu makubaliano na kuwapa taarifa

DIGNITY Kwanza
Human Dignity and Inclusive Development

## TIMU YETU

**Mkurugenzi Mtendaji.**
Janemary Ruhundwa

**Huduma za kisheria na utetezi**
Mwajabu Khalid

**Uwezeshaji Jamii na mipango ya Maendeleo**
Jovin Sanga

**Utawala na Fedha**
Rashid Haji Nyembo

**Afisa mipango – Sheria na Ushawishi**
Bishara Msallam

**Afisa mipango – Sheria, utetezi na mawasiliano.**
Faith Mario Mjalilla

**Afisa Miradi**
Joan Kyabemela

Timu ya watu wa kujitolea.

## TUNAPATIKANA :

Nyumba na. 13,mtaa wa Vinyaji,Karibu na barabara ya Cocacola kutoka kituo cha Bajaj Osama
Mikocheni B, Dar es Salaam
S.L.P 33035 Dar es Salaam;
Simu +255 22 27 81 176; au +255 788 609 094
Email: info@dignitykwanza.org;
Website: www.dignitykwanza.org

## WASIFU



DIGNITY Kwanza
Human Dignity and Inclusive Development

# DIGNITY KWANZA UTU NA MAENDELEO



## HISTORIA

**DIGNITY Kwanza-Community Solutions**, ni shirika lisilo la kiserikali ambalo limesajiliwa hapa Tanzania chini ya sheria ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2005. DIGNITY Kwanza ilianzishwa na kikundi cha watu binafsi ambao walikuwa wanafanya kazi katika shirika la Asylum Access Tanzania (AATZ) ambalo lilikuwa linafanya kazi Tanzania na kusitisha shughuli zake mwezi Juni mwaka 2018.

**DIGNITY Kwanza** ilianzishwa ili kuweza kuendeleza huduma ambazo zilikuwa zikifanywa na AATZ kama, huduma ya kisheria, kuinua jamii kwenye maswala ya kiuchumi na maisha katika jamii. DIGNITY Kwanza haitaendelea kuhudumia wakimbizi tu bali itahudumia pia jamii ya makundi yaliyo katika mazingira hatarishi na wasiojiweza.

## MAONO

Tunaiona Tanzania ni sehemu ambayo mtu anaishi kwa utu na uhakika wa kupata fursa ambayo itamuwezesha kujikimu na kuchangia maendeleo katika kujenga taifa.

## DHAMIRA

Dhamira yetu ni kulinda na kukuza utu wa binadamu kwa makundi yaliyotengwa na yanayoishi katika mazingira magumu kuwapa maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia elimu, misaada na uwezeshaji.

## MALENGO

1. Kukuza na kuendeleza fursa kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kwenye kukua kiuchumi.
2. Kushawishi ukuzaji na ulinzi wa haki za binadamu kwa makundi yaliyoko pembezoni na yanayoishi katika mazingira magumu nchini Tanzania
3. Kuwezesha kupata msaada wa kisheria kwa makundi ya watu waishio katika mazingira hatarishi na yaliyo pembezoni
4. Kushawishi serikali na jamii katika kupunguza hali ambazo zinaletea uhatarishi na mazingira magumu kwa makundi mbalimbali mfano; wakimbizi kutegemea msaada, ukosefu wa ajira kwa vijana, kutokuwa na usawa wa kijinsia, unyayasaji wa watoto.
5. Kukuza na kutetea utawala bora, uwajibikaji, uwazi, amani, na usalama kama msingi wa utu wa ubinadamu na maendeleo kwa ujumla.
6. Kukuza afya, elimu, na ustawi kwa ujumla wa watu waliotengwa na watu walio pembezoni

## WALENGWA

1. Wakimbizi, waomba hifadhi, wahamiaji walio katika mazingira hatarishi.
2. Watu wasio na utaifa na watu walio katika hatari ya kukosa utaifa.
3. Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri (na uangalizi maalum kwa wanawake, watoto na vijana)





## HUDUMA TUNAZOTOA

1. Msaada wa kisheria kwa mtu mmoja mmoja na makundi (ushauri wa kisheria, elimu na uwakilishi)
2. Uwezeshaji wa jamii na msaada
3. Misaada ya kibinadamu na ya kimaendeleo
4. Utetezi, kukuza uelewa na ushawishi

## MAENEO YETU MAKUU YA KIMKAKATI

1. Hadhi ya kisheria
2. Haki ya kiuchumi na kijamii
3. Usawa wa kijinsia
4. Utawala Bora na uwajibikaji

## NINI KILICHOPO KWENYE JINA?

Utu na maendeleo ni pande mbili za sarafu moja. Wakati kila mtu katika jamii anaweza kuishi kwa kuheshimiwa utu wake, maendeleo yake kijamii na kiuchumi ni muhimu yazingatiwe.

Kwa bahati mbaya imekuwa ni kawaida hususani katika nchi zinazoendelea kutenganisha dhana hizi mbili. Mipango na miradi ya kimaendeleo itengenezewe mikakati ya kuheshimu, kulinda na kuthibitisha utu kwa kuwa utu ndiyo nguzo ya maendeleo. Kutokuwepo kwa mikakati hiyo kunapelekea makundi ya watu waishio katika mazingira magumu na hatarishi kukumbwa na matatizo kama uvunjifu wa haki za msingi,